**JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YASONGWE**

**SHULE YA SEKONDARI MAWENI,**
**S.L.P 111, MKWAJUNI-SONGWE.**
**TAREHE 23 /04/2024**

**Namba ya simu;**
**Mkuu wa shule ….0759-007583**
**Makamu mkuu wa shule …0753 005 884**
**Matron …. 0767373618**
**Patron……0766027090**
**MAWENI BLOGS; mawenisecondary.blogspot.com**

**KUMB NA.SDC/ MWN/ ADM/VOL.I/15.**
**Mzazi/mlezi wa mwanafunzi………..**
**S.L.P………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAWENI KWA MWAKA WA MASOMO 2024/2025**

1. Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kukupongeza kwa kufaulu Mtihani wako wa Kidato cha Nne, kitendo ambacho kimekuwezesha kujiunga na na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya Maweni kwa mwaka wa masomo **2024/2025** tahasusi ya……………… Ni matumaini yangu kwamba bahati hii utaitumia vizuri kwa namna yeyote ile ili uweze kutimiza ndoto zako, za shule na taifa kwa ujumla.

Aidha ni tegemeo langu pia kuwa utakuwa na nidhamu nzuri na utatekeleza na kufuata Sheria, taratibu na kanuni zote za shule kama utakavyoelekezwa.

## MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Maweni ipo umbali wa kilomita 1.5 magharibi mwa stendi kuu ya mabasi ya Mkwajuni katika **Mkoa wa songwe wilaya ya songwe**. Ili uweze kufika kwa urahisi fika stendi kuu ya mabasi ya mbeya, kisha panda mabasi madogo maarufu kwa jina la mzunguko yaendayo mbalizi (Tarafani) na nauli ni shilingi mia saba (700/=) tu, hapo utakuta mabasi yaendayo mkwajuni/Songwe na nauli ni shilingi elfu nane (8,000/=)tu.

Kwa kawaida mabasi hayo yanapatikana kuanzia saa tatu asubuhi, hadi saa tisa alasiri, utashukia stendi ya mkwajuni maarufu kwa jina la stendi mpya na hapo utapata bodaboda au bajaji kwa shilingi elfu mbili tu (2,000/=) tu mpaka shuleni.

Ndugu mzazi, muhula wamasomo utaanza tarehe **…………………**hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe**……………..**usiporipoti kwa wakati nafasi yako itachukuliwa na mwenzako ambaye hajapata nafasi.

**2. MAMBO MUHIMU YAKUZINGATIA:-**

**2.1 SARE ZA SHULE.**

**A. Wasichana**

I. Shati mawili (2) rangi nyeupe tetroni mikonomirefu.
II. Brazia nyeupe au nyeusi
III. Sketi mbili **NDEFU** (2), light blue na dark blue. Mshono ni kama inavyoonekana kwenye picha. Tazama kiambatisho Na.5

- Nguo ya kushindia ni gauni la rangi ya dark blue mshono ni solo, iwe ndefu ya kutosha.

IV. Viatu vyeusi vya kamba naviwe na kisigino kifupi jozi mbili (2).
V. Soksi nyeupe jozi mbili (2) auzaidi.
VI. Sweta mbili, rangi ya light Blue na dark blue shingo yaV.
VII. T-shirt ya dark blue muundo wa form six
VIII. Kwa msichana wa kiislamu hijabu nyeupe inaruhusiwa ifunike kifua pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
X. Nguo za michezo rangi ya light blue/dark blue na rabanyeupe/nyeusi
XI. Tracksuit rangi light blue ni lazima iwe pana ya kutosha.
XII. Begi la kubebea madaftari “School Bag” rangi Nyeusi.
XII. Tai mbili ndefu, light blue na darkblue.

**b). Wavulana**.

i) Shati mbili rangi nyeupe tetron mikono mirefu.
Suruali mbili2 za **HESHIMA** ,rangi light blue na darkblue,kama inavyoonekana kwenye picha**. Tazama kiambatisho Na. 5**
ii) Viatu vyeusi jozi mbili viwe na kisigino kifupi na pia viwe vya kamba.
iii) Soksi jozi mbili au zaidi ranginyeusi/brown
iv) Sweta mbili 2, light blue na dark blue shingo ya V.
v) Nguo za kushindia, suruali rangi nyeusi isiyobana.
vi) T-shirt ya dark blue muundo wa form six
vii) Tracksuti rangi ya dark blue.
viii) Nguo za michezo rangi ya light blue/ dark bluena rabanyeupe/nyeusi.
ix) Begi jeusi la kubeamadaftari.
x) Tai mbili ndefu light blue na darkblue.

**2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI**

I. Daftari 10 (Quire 3).

II. Ream (A4) bunda mbili anaporipoti shuleni
III. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika, orodha imeambatishwa.
IV. Dissecting kit kwa wanafunzi wanao soma Biology.
V. Scientific calculator.
VI. Godoro ft 2.5
VII. Mashuka jozi mbili rangi ya pink na light blue, blanket jepesi moja, foronya ya godoro mbili rangi ya pink na light blue, mto mmoja na chandarua moja rangi ya light blue au nyeupe.
VIII. Nguo za ndani za kutosha
IX. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko, dumu lita tano la kutunzia maji safi ya kunywa na kikombe)
X. Ndoo mbili za lita ishirini kwa ajili ya kutunzia maji zenye mifuniko.
XI. Kwanja 1, jembe 1, mopper 1, mifagio 2 wa ndani na wa nje.
XII. Taulo, Mswaki, Sabuni, mafuta n.k
XIII. Fedha zake za matumizi binafsi.
XIV. Pasi ya Mkaa kwa ajili ya kunyoshea nguo inaruhusiwa.
XV. Tranka (Sanduku la chuma/ bati) kuwekea vifaa vyake.

**2.3 MICHANGO MBALIMBALI ANAYOTAKIWA KULIPA MWANAFUNZI;**

| NA | MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo ya shule | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

Jumla kuu tajwa hapo juu ilipwe kweny**e akaunti namba 60706600135 NMB BANK**, jina la akaunti ni**Maweni Sekondari** (kumbuka kuandika jina la mwanao kwaenye bank paying slip kwa matumizi ya ofisi

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE KWA WANAFUNZI WOTE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Raisi – **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule kama vile school baraza, kupandisha bendera, kushiriki katika michezo, subject clubs na vipindi vya dini.
iii. Kushiriki kwa ukamilifu masomo ya jioni.
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule au shamba dress wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, matron ama patron; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Kuitika miito ya dharura maramoja
xiii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni **(MWANAFUZI ATANYOA NYWELE KATIKA SALOON YA SHULE TU** ni marufuku kunyoa nywele nje yashule).
xiv. Kuheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Serikali na Nembo yaTaifa
xv. Kuheshimu taratibu za Mikutano, Ofisi za Shule, mali ya binafsi na mali yaumma
xvi. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani au nje ya shule.

**MUHIMU**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni Kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule (Msiba au ugonjwa).**

## 3.2. MAKOSA YANAYO WEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule;
vi. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau bendera ya taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k na;
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 3.3 AFYA

Wagonjwa wote watapata kibali cha kwenda Hospitali kupitia Ofisi ya malezi au mwalimu wa afya. Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na**kadi ya bima** ya afya ili kupunguza gharama za matibabu Endepo mwanafunzi hana bima ya afya.

## 3.4. USAFI

Usafi ni jukumu la kila mwanafunzi kama sehemu ya maisha yake ya kila siku, hivyo utashughulikia;

a) Usafi binafsi wa mwili na mavazi yako
b) Usafi wa maeneo kama utakavyopangiwa; ukumbi wa chakula/jikoni, mabweni, vyoo, madarasa, maabara, viwanja nabarabara.
c) Vyakula viliwe sehemu husikatu.

Wageni wa wanafunzi wakati wapo Shuleni lazima waonane kwanza naMwalimu wa zamu/wa Darasa/Bweni au Matroni ambaye amepewa uwezo wa kukubali au kutokubali kuonana naMwanafunzi.

Huruhusiwi kuja na vitu vifuatavyoshuleni;

a) Simu ya mkononi
b) Pasi ya umeme
c) Nguo zisizo zashule

**NB**

Ukija navyo utarudisha nyumbani

## 3.5 MASHARTI YA KUJIUNGA NA BWENI

Pamoja na sheria na kanuni muhimu za shule unapaswa;

1. Kukubaliana na sheria na kanuni zote zashule
2. Kufuata ratiba ya siku kwa mwanafunzi wa bweni
3. Kuhudhuria **"Roll-calls"** zote kama inavyopangwa nawalezi
4. Kuhudhuria **"Preps"** na vipindi vyote vyadarasani
5. Kuishi kwa amani, upendo na ushirikiano wa kidugu na wanajumuiyawote
6. Kula **"Menu"** iliyoandaliwa na Shule bila kuleta usumbufu wa kujichaguliachakula.

7. Kuchangia gharama za matengenezo ya uharibifu wowoteinapolazimu.
8. Kutomleta au kumwingiza mgeni yeyote ndani ya bweni (wanafunzi wa kutwa ni miongonimwao)
9. Kutoleta au kukaa ndani ya bweni bila ruhusa ya walezi wakati wamasomo
10. Huruhusiwi kupikachochote
11. Ni marufuku kwa wanafunzi wavulana kuingia bweni lawasichana
12. Kutokulala nje ya Shule bila kibali cha **Mkuu washule**
13. Kutoka nje ya shule bila kibali maalumu cha**utawala**
14. Kuvaa sare ya shule wakati wote wa vipindi na awapo nje ya mipaka ya shule. (kwa shughuli binafsi, shule aukidini)
15. Kuvaa sare ya nje (shamba dress) baada ya saa za masomo ndani ya mipaka ya shule.
16. Zingatia. Unaruhusiwa kuabudu kwa kadri ya dini yako ila usivunje sheria na taratibu zilizowekwa hapa shuleni.

**4. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5\. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**.................................**
**LEONARD MPOLI**
**Mkuu wa Shule**

**MAWENI S.S**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule ………0759007583**
- **Makamu Mkuu wa Shule ……0753005884**

- **Mwandamizi Taaluma ………0620201106**

- **Mwandamizi Malezi …………0766027090**

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

**1.** Mimi……………………………………………………..nina kubali mtoto wangu…………………………………….wa kidato cha …….……mwaka ……… kujiunga na sekondari ya Maweni kuanzia tarehe……………………… akiwa mwanafunzi wa bweni.

**2.** Ninakubali masharti yaliyomo katika kujiunga na bweni ikiwa ni pamoja na kulipa karo yote ya shule na kumtimizia mahitaji mengine yashule.

**3.** Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa na afya isiyoridhisha ambayo itahitaji ukaribu wa matunzo ya mzazi /mlezimwenyewe.

**4.** a) Anuani yangu ya kudumuni
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
……………………………….........................................................................

b) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao zasimu
ni
1……………………………………………………………………………..
2 ……………………………………………………………………………..
3 ………………………………………………………………………………
4………………………………………………………………………………

c) Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekelezakikamilifu.

**5.** Sahihi ya mzazi /mlezi……………………………………..tarehe……………

**FOMU YA KUKUBALI (FOMU HII IRUDISHE SHULENI)**

**1.** Mimi……………………………………………...kidato cha………nimekubali kujiunga na shule ya sekondari Maweni nikiwa mwanafunzi wabweni.

**2.** Ninakubali masharti yote, nina ahidi kufuata sheria zote zashule.

**3.** Niko tayari uongozi wa shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi endapo nitakiuka mashartiyaliyomo.

**4.** Sahihi yamwanafunzi………………………………….tarehe………………

*Kiambatisho Na. 2*

## FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI

**1.** Jina kamili…………………………………………………………………………

**2.** Mahali ulipotokea.…………………………………………………………..

**3.** Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………

**4.** Uraia…………………………………………………………………………

**5.**Anuani ya nyumbani……………………………………………..………..

**6.** Jina la mzazi /mlezi………………………………………………………..

**7.** Anuani ya mzazi/mlezi (kama tofauti na hiyo hapojuu)…………………..

……………………………………………………………………………………..

**8.** Ndugu wa karibu. Anuani yake, kitongoji/mtaa……………………………

| Jina | Uhusiano | Anuaniyake | Simu |
|---|---|---|---|
| 1……......................... | ………............ | ……………….. | ……………..... |
| 2................................. | ..................................................... | | …................ |
| 3................................. | ............................. | .......................... | ……............... |
| 4................................. | .............................. | ........................... | ….................. |

9. Dini...........................................................................................................................

10. Kidato alichopokelewa..........................................................................................

**11**. Shule uliyotoka……………..............................................................................

**12**. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba, n.k..........................................................................................

**13.** Wilaya unakotoka……...................... mtaa……………….. kata………..............

**14**. Sahihi ya mwanafunzi…………………………………….. tarehe…………………

**15**. Sahihi yamzazi/mlezi……………………………………….tarehe………………..

**Matumizi ya ofisi**

**Namba ya**

**shule**……………………………………………………………………..**Namba ya**

**mtihani**………………………………………………………………..

*Kiambatisho Na. 3*

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION MAWENI SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 111 MKWAJUNI SONGWE**

To be completed by medical officer.
Full name………………………………………………………………………………
Age………………………Years……………………………Sex…………………….…
Blood count (Red and White)…………………………………………….............
Stool examination………...............................................................................
Urine analysis…………………………………………………………………………
Syphilis test……………………………………………………………………………
Eye test………………………………………………………………………………..
T.B test………………………………………………………………........................
Ears…………………………………………………………………………………..
Chest…………………………………………………………………………………
Spleen………………………………………………………………………………..
Abdomen……………………………………………………………………………
**ADDITIONAL INFORMATION** e.g. physical or chronically familydisease, etc………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

I certify that the above named student is fit to peruse studies
Signature………………………………………………………………………
Designation……………………………………………………………………
Section…………………………………………………………………………..
Date……………………………………………………………………………………

**NOTE**: Medical officer at the time of examination the individual for any aliments you note.

**PUPILS:**
You must bring this complete form when you come to school, no pupil may enroll without certificate of physical fitness

…………………………
LEONARD MPOLI
MKUU WA SHULE

*Kiambatisho Na. 4*

**MAWENI SECONDARY SCHOOL**
**ESSENTIAL REFERENCE BOOKS/TEXT BOOKS FOR A-LEVEL STUDENTS.**

## A.HISTORY

**1.** Major issues in AfricaHistory-ICD
**2.** Major Events in AfricaHistory-Mwaijage
**3.** The Political Economy, Imperialism-byNabudere
**4.** Africa since 1800-4th edition-by Roland Oliver andAtmore
**5.** The making of modern Africa Vol.1
**6.** How Europe underdeveloped Africa-W.Rodney
**7.** The 20th century –byDuff.M.N
**8.** Europe from 1815 –byPeacock

## B.GEOGRAPHY

**1.** Certificate Geography (Oxford) Form 3-by Mary Mugo, Robert Karuggah and Paul Kibuuka.
**2.** General Geography in diagrams –byR.B.Bunnet
**3.** Regional Geography-byNyambali/Nyangwine
**4.** Photography Interpretation and Elementary Surveying for Secondary Level New Edition-by S.E.Dura
**5.** Certificate Human and Economics Geography-by Morgan and LeongChang

## C.KISWAHILI

### USHAIRI
**1.** Kimbunga-G.Gora (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili –TUKI)1994
**2.** Chungu Tamu-T.A.Mvungi. (Tanzania Publisher House)1985
**3.** Mapenzi Bora-S.Robert (Mkuki na Nyota)2003
**4.** Fungate ya Uhuru-M.S. Khatibu (Macmillan andAidan)

### RIWAYA
**1.** Vuta n'Kuvute-Shafi .A.Shafi (Mkuki naNyota)1999
**2.** Kufikirika –S.Robert (Mkukin a Nyota)2003
**3.** Mfadhili –Hussein Tuwa (Mathew B/W and Stationery)2007
**4.** Usiku utakapokwisha- Mbunda Msokile (Macmillan and Aidan)2007

### TAMTHILIYA
**1.** Morani-E.Mbogo(DUP)
**2.** Kivuli kinaishi-Said Mohamed (Oxford University Press)2007
**3.** Kwenye Ukingo wa Thim-E.Hussein (UniversityPress)
**4.** Nguzoya Mama-DUP (1982)

**D. GENERALSTUDIES**

1. General Studies (Communication Skills for A-Level –M.Kadeghe)
2. General Studies notes (for A-Level Fir V & VI) G. Mshiu and N.Nyagwine

**E. ENGLISHLANGUAGE**

1. A Complete course for Form V & VI –MichaelKadeghe
2. English for Form V &VI – by MichaelKadeghe
3. Teaching English as a Foreign Language – G. Broughton et.Al
4. A grammar of Contemporary English – Quirk, et.Al
5. Longman English Grammar- L. GAlexander
6. The real English textbook for Advanced Level- by M.Kadeghe
7. Advance EnglishDictionary

**PART II**

**A.**

**NOVEL**

1. The Beautiful One Are Not Yet Born- A. KAmah
2. A Man of the People – C.Achebe
3. Divine providence- Mkuki naNyota
4. Encounters from Africa – Macmillan
5. The Rape of the Peal-Macmillan

**B. PLAYS/DRAMA**

1. An Enemy of the People – H.Ibsen
2. I will marry when I want-EAEP
3. Rwanda Magere- by Okot Omtatah (1991)- Heinemann,Kenya
4. The Bride –EAEP
5. Black Mamba – EAEP

**C. POETRY**

1. Selected Poem from institute ofEducation
2. The Wonderful Surgeon and other Poem – Mkuki naNyota

**D. ECONOMICS**

1. AMBILIKILE – NEW SYLLABAS-200
2. MORDEN ECONOMIC –ROBERT MUDIDA
3. ECONOMIC I ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010SYLLABUS
4. ECONOMIC II ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010SYLLABUS
5. ECONOMIC A/LEVEL PAPER I AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M.AMBIKILE NEW+SYLABUS
6. ECONOMIC A/LEVEL PAPER II AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M.AMBIK

***Kiambatisho Na. 5***

SARE ZA SHULE

**A 1. WASICHANA**



A2 WASICHANA WAISLAMU ( DARK & LIGHT )



B. WAVULANA



C. SHAMBA DRESS WASICHANA

